AfCHPR
African Court on Human and Peoples' Rights

Arusha, Tanzania
Tovuti: www.african-court.org
Simu: +255-27-970-430

**MUHTASARI WA HUKUMU**

**LAMECK BAZIL DHIDI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAOMBI NA. 027/2018**

**HUKUMU KUHUSU UZINGATIAJI WA SHERIA NA FIDIA**

**TAREHE 13 NOVEMBA 2024**

**UAMUZI WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU**

**Arusha, tarehe 13 Novemba 2024**: Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama), imetoa hukumu katika kesi ya *Lameck Bazil dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*.

*Lameck Bazil* (Mleta Maombi) ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mjibu Maombi). Wakati wa kuwasilisha Maombi haya, alikuwa amefungwa katika Gereza Kuu la Bukoba mjini Bukoba, baada ya kukutwa na hatia ya mauaji na akahukumiwa kifo kwa kunyongwa. Mleta Maombi alidai kwamba Mjibu Maombi alikiuka haki zake za kusikilizwa kwa haki, zinazolindwa chini ya Kifungu cha 7 cha Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu (Mkataba), kwa kumhukumu kwa misingi ya ushahidi unaopingana kutoka kwa mashahidi wa upande mashtaka na kupitia kushindwa kwa upande mashtaka kuthibitisha ushahidi wake bila shaka yoyote. Alitaka apewe fidia ili kufidia ukiukaji huu unaodaiwa kufanywa.

Mahakama iliona kwamba, kwa mujibu wa Kanuni ya 63(1) ya Kanuni za Mahakama, ina mamlaka ya kutoa hukumu moja kwa moja, ama kwa kuombwa na Mleta Maombi au kwa hiari yake, ikiwa masharti yaliyomo katika Kanuni ya 63(1) ya Kanuni za Mahakama yalitimizwa. Katika kesi hii, hukumu ya moja kwa moja iliyolewa kwa uamuzi wa Mahakama, kwani Mahakama iliridhika kwamba Mjibu Maombi alikuwa amepewa hati zote zinazohusiana na kesi; na kwamba Mjibu Maombi alikuwa amekosea kwa kushindwa kuwasilisha Majibu yake.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 3 cha Itifaki ya Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu kuhusu Kuanzishwa kwa Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Itifaki), Mahakama ilipaswa kwanza kuamua endapo ilikuwa na mamlaka ya kusikiliza Maombi hayo. Katika suala hili, Mahakama ilibaini kuwa ilikuwa na mamlaka binafsi kwani, tarehe 29 Machi 2010, Mjibu Maombi iliweka Azimio lililotolewa chini ya Kifungu cha 34(6) cha Itifaki ambacho kinaruhusu watu binafsi kuwasilisha maombi dhidi ya Mjibu Maombi

kulingana na Kifungu cha 5(3) cha Itifaki. Mahakama ilisisitiza kwamba Mjibu Maombi kuondoa Azimio hilo, mnamo tarehe 21 Novemba 2019, hakukuathiri Maombi haya kwani uondoaji huo ulianza kutekelezwa mnamo tarehe 22 Novemba 2020, ambayo ilikuwa tarehe baada ya Maombi haya kuwasilishwa, mnamo tarehe 22 Oktoba 2018.

Mahakama iliona kwamba ilikuwa na mamlaka ya kisheria kwa sababu Mleta Maombi alikuwa amedai haki zake, zinazolindwa chini ya Mkataba zilikiukwa. Aidha, Mahakama iliona kwamba ilikuwa na mamlaka ya muda kwa kuwa ukiukaji unaodaiwa ulitokea baada ya Mjibu Maombi kuwa mhusika wa Itifaki. Mwisho, ilibaini kuwa ilikuwa na mamlaka ya kieneo, ikizingatiwa kuwa ukweli wa jambo hilo ulitokea ndani ya eneo la Mleta Maombi.

Mahakama iliona kwamba kwa mujibu wa Kifungu cha 6(2) cha Itifaki, ambacho maudhui yake yamerudiwa katika Kanuni ya 50(1) ya Kanuni za Mahakama, lazima iamue kuhusu ukubalifu wa kesi zilizowasilishwa mbele yake. Kwa hivyo, Mahakama iliona kwamba, kwa mujibu wa Kifungu cha 50(2) cha Kanuni za Mahakama, Maombi haya yalikuwa yametimiza masharti ya ukubalifu yafuatayo: Mleta Maombi alikuwa ametambuliwa kwa udhahiri kwa jina katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(a) ya Kanuni za Mahakama. Iliona pia kwamba madai ya Mleta Maombi yalilenga kulinda haki zake kulingana na Kifungu cha 3(h) cha malengo ya Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika, na hivyo Maombi yalizingatia Kanuni ya 50(2)(b) ya Kanuni za Mahakama. Aidha, Mahakama ilibaini kwamba lugha iliyotumika katika Maombi haikuwa ya dharau au ya matusi kwa Mjibu Maombi au taasisi zake katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(c) ya Kanuni za Mahakama. Maombi haya pia hayakutokana tu na habari zilizosambazwa kupitia vyombo vya habari, katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(d) ya Kanuni za Mahakama.

Kuhusu kukamilisha taratibu za ndani, Mahakama ilibaini kuwa Mleta Maombi alikuwa amekata rufaa kwenye Mahakama ya Rufaa, ambacho chombo cha juu cha mahakama ya Mjibu Maombi, uamuzi wa Mahakama Kuu kumtia hatiani kwa mauaji kwenye Mahakama ya Rufaa. Mahakama ya Rufaa ilitoa uamuzi wake tarehe 4 Septemba 2018, ikitupilia mbali rufaa ya Mleta Maombi. Kwa hivyo, Mleta Maombi alikuwa amekamilisha taratibu za ndani kwa kuzingatia Kanuni ya 50(2)(e) ya Kanuni za Mahakama. Mahakama iliona pia kwamba Maombi yalikuwa yamewasilishwa mbele ya Mahakama kwa wakati unaofaa, wa mwezi mmoja na siku 18 baada ya uamuzi wa Mahakama ya Rufaa kutolewa tarehe 4 Septemba 2018. Kwa hivyo, Maombi haya yalikuwa yamezingatia Kanuni ya 50(2)(f) ya Kanuni za Mahakama. Mahakama pia ilijiridhisha kwamba Maombi haya hayakuibua madai ambayo tayari yalisuluhishwa mbele ya mahakama nyingine ya kimataifa. Matokeo yake, Mahakama ilitangaza kuwa Maombi hayo yanakubalika.

Kuhusu uzingatiaji wa sheria wa kesi hiyo, Mahakama iliangalia endapo Mjibu Maombi alikiuka haki za Mleta Maombi chini ya Kifungu cha 7(1) cha Mkataba, kwa kudaiwa kumhukumu kwa misingi ya taarifa zinazopingana za mashahidi wa upande wa mashtaka na kwa kushindwa kwa upande wa mashtaka kuthibitisha kesi yake bila shaka yoyote. Katika suala hili, Mahakama iliona kwamba jinsi kesi za ndani zilivyoendeshwa zilifuata viwango vya kimataifa, na kwa hivyo madai ya ukiukaji wa haki ya mtu kusikilizwa kwa haki, inayolindwa chini ya Kifungu cha 7 cha Mkataba, yalitupiliwa mbali.

Ingawa Mleta Maombi hakudai ukiukaji wa haki yake ya kuishi inayolindwa chini ya Kifungu cha 4 cha Mkataba, Mahakama kulingana na busara yake ya kisheria iliona kuwa kutolewa kwa adhabu ya kifo ya lazima kulizuia utekelezaji wa busara ya mahakama, kwa upande wa afisa wa mahakama. Kwa hivyo, Mahakama iliona kwamba haki ya Mleta Maombi ya kuishi ilikuwa imekiukwa.

Vivyo hivyo, Mleta Maombi hakuonesha haki yake ya utu ilikuwaimekiukwa, hata hivyo, Mahakama ilisisitiza uamuzi wake wa kisheria unaoonesha kwamba utekelezaji wa hukumu ya kifo kwa kunyongwa ni ukiukaji wa haki ya utu kama inavyolindwa chini ya Kifungu cha 5 cha Mkataba.

Mahakama, baada ya kugundua ukiukaji wa Kifungu cha 4 na 5 cha Mkataba, iliamuru Mjibu Maombi achukue hatua zote muhimu, ndani ya kipindi cha mwaka mmoja baada ya kutolewa taarifa ya hukumu, aondoe utoaji wa hukumu ya kifo ya lazima kwenye sheria zake; aondoe hukumu ya Mleta Maombi, ndani ya kipindi cha mwaka mmoja baada ya taarifa ya hukumu kutolewa na kusikiliza upya kesi yake kuhusu kutoa hukumu, kupitia utaratibu ambao unaruhusu kutumia busara ya mahakama.

Aidha, iliamuru Mjibu Maombi achukue hatua zote muhimu za kuondoa kunyonga kwenye sheria zake, kama njia ya kutekeleza hukumu ya kifo ndani ya miezi sita baada ya kupokea taarifa ya hukumu hii; na kuchapisha hukumu hii ndani ya kipindi cha miezi mitatu tangu tarehe ya kupokea taarifa.

Kila upande uliamriwa kubeba gharama zake.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 70(3) ya Kanuni za Mahakama, Jaji Blaise Tchikaya na Jaji Dumisa B. Ntsebeza walitoa Maazimio kuhusu suala la adhabu ya kifo.

**Maelezo zaidi**

Maelezo zaidi kuhusu kesi hii, ikiwa ni pamoja na hati kamili ya uamuzi wa Mahakama ya Afrika, inaweza kupatikana kwenye tovuti kwenye: https://www.african-court.org/cpmt/details-case/0272018.

AfCHPR
African Court on Human and Peoples' Rights

Arusha, Tanzania
Tovuti: www.african-court.org
Simu: +255-27-970-430

**MUHTASARI WA HUKUMU**

Kwa maswali mengine yoyote, tafadhali wasiliana na Msajili kwa barua pepe registrar@african-court.org.

*Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ni mahakama ya bara zima iliyoanzishwa na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika ili kuhakikisha haki za binadamu na watu barani Afrika zinalindwa. Mamlaka ya Kisheria ya Mahakama kuhusu kesi na mizozo yote iliyowasilishwa kwake kuhusu tafsiri na utekelezaji wa Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu na chombo kingine chochote cha Haki za Binadamu kilichoidhinishwa na Nchi zinazohusika. Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu www.african-court.org.*

.